

# Pambazuko

Toleo Namba 34

Jumatatu Aprili 10-16, 2023

## Kesi ya Yesu ilivunja sheria

Uk.16



# Kuna viongozi wabovu 747

● Ni katika halmashauri

Uk. 10

Balozi Karume amvaa Dkt. Mwinyi

Uk. 5

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye  
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

**Salamu**

## Heri ya Pasaka

*Uongozi wa Gazeti la Pambazuko,  
waandishi wa habari na wachangiaji  
wake, wanapenda kuwatakia heri ya  
Jumatatu ya Pasaka wasomaji wake  
wote walioko  
maeneo mbalimbali  
ya dunia.*

*Katika kuwatakia  
heri hiyo, Gazeti  
la Pambazuko  
linapenda kuhimiza  
kudumishwa kwa  
upendo, ushirikiano  
na uaminifu katika  
kumtumikia Mama  
Tanzania na  
watoto wake -  
wananchi.*

*Pasaka  
Njema*



# BABA NA MWANA...



Rais (mstaafu) Jakaya Mrisho Kikwete, kulia, akiteta jambo na mwanaye, Ridhiwani Kikwete ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ridhiwani, mwanasheria, anaonekana kufuata nyayo za baba yake - hatua kwa hatua na ngazi anayopanda ni kama ilele aliyotumia baba yake kumfikisha kwene ukuu zaidi. Siku za usoni Pambazuko italeta ngazi na hatua hiso. (Picha kutoka maktaba).

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya WhatsApp: **+255 744 768263** kwa kutuma neno "**HABARI**" kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwene WhatsApp yako.
- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kuitia email yako, andika neno "**HABARI**" na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



"Serikali inafanya kila linalowezekana kuwapa elimu, lakini uamusi wa kuitumia elimu hiyo ni wenu, tambueni kuwa upo mzigo mkubwa sana wa kuongoza hii nchi unawasubiri, someni kwa bidii sana, mpate maarifa na ufahamu mkubwa. Msituangushe" - Benjamin William Mkapa, Rais wa Tanzania (1995 – 2005). Mkapa sasa ni marehemu.

## Tafakuri

### Nadhairia murua, Dira ya Taifa bora

**Na Deusdedith KAHANGWA**

**A**PRILI 3, 2023, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango, alizindua mchakato wa maandalizi ya Dira ya Tanzania ya Maendeleo Kuelekea 2050.

Uzinduzi huo ulifanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Dkt. Mpango alisema kuwa, kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana kupitia Dira ya Tanzania Kuelekea 2025, Dira ya Tanzania Kuelekea 2050 inatarajiwa kuwa nyenzo ya kuleta ustawi kwa kila raia.

Hivyo, Dkt. Mpango aliwataka wadau wote wa maendeleo kushiriki katika mchakato huo kwa kutoa maoni na taarifa kwa timu ya maandalizi, ili iweze kufanya uchambari wenye halisia na utoshelevu.

Dira ya Tanzania ya 2025 inayotegemewa kumalizika mwaka 2025 ilizinduliwa mwaka 1999.

Inaelezwu kuwepo kwa mema na mabaya katika utekelezaji wa Dira ya Tanzania Kuelekea 2025. Mabaya yaliyifanya Dira ya Tanzania Kuelekea 2025 isifanikiwe Kikamilifu.

Malengo makuu ya Dira ya Tanzania 2025 ilikuwa ni kufikia uchumi wa kati na kuwa na taifa lenye hali bora ya maisha kwa watu; amani, umoja na utulivu; uongozi bora; jamii iliyoelimika na uchumi wenye ushindani.

Kwa mujibu wa Dkt. Mpango, tathmini ya utekelezaji wa Dira ya 2025 inaonyesha kuwa, pamoja na kipato cha Watanzania kuongezeka, bado asilimia 26.4 ya Watanzania wanaishi chini ya kiwango cha mstari mwekundu wa umaskini.

Katika jicho la uchambari na upekuzi wa kimantiki, Dira ya Tanzania Kuelekea 2025 inaonyesha kwamba kuna dosari kubwa mbili zilizoifanya isifanikiwe kwa ukamilifu.

Kwanza, andiko la kwanza la Dira ya Tanzania Kuelekea 2025, la mwaka 1999, halikuwa na vigezo vyaa kupima kasi ya ufanisi.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango,*

Dosari hii ilizibwa mwaka 2015, kwa kuandika "kiambatanisho" kilichoitwa "Long Term Perspective Plan."

Kutokana na uzoefu huu, sasa Zanzibar tayari wanayo Dira ya Zanzibar Kuelekea 2050, yenye kutaja vigezo vyaa kupima kasi ya ufanisi kwa kila sekta iliyotajwa ndani yake.

Na pili, Dira ya Tanzania Kuelekea 2025 haikutokana na nadhairia mbaya ya kusanifu mipango mikakati. Badala yake iliandikwa kwa mtindo ambao unawenza kuitwa 'fomati huru.'

Dosari hii iliifanya mipango ya maendeleo ya muda mfupi iliyoandalialiwa kwa ajili ya kuitafsiri Dira ya Tanzania kukosa mwongozzo thabiti wa kinadharia. Dira ya Zanzibar Kuelekea 2050 hajiaweza kuepuka dosari hii.

Kwa hiyo, ni mwito kwamba, maandalizi ya Dira ya Tanzania Kuelekea 2050, yaepuke makosa haya mawili. Kuhusi nadhairia ya kusanifu mipango kikakati itafaa zaidi ikiwa nadhari inayoitwa "Balanced Score Card Framework (BSC)," itapewa nafasi.

Mfumo wa BSC utawezesha kuandaan mpango mkakati unaoonyesha rasilimali, sekta za utekelezaji, walengwa, shabaha, dira, dhima na vigezo vyaa kupima ufanisi kwa kila sekta.

## Balozi Karume amvaa Dkt. Mwinyi

Na Mwandishi WETU,  
Unguja

**H**ATUA ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kukodisha visiwa vidogo, inaendelea kuwa na ukakasi.

Wapo baadhi ya watu wanaoona hatua hiyo, pamoja na Dkt. Mwinyi kueleza mara kadhaa kwamba lengo kubwa ni kupata fedha kwa ajili ya maendeleo ya Wazanzibari, ni kuhatarisha zaidi ustawi wa umma.

Kwamba kukodisha visiwa hivyo hakuna tija kwa umma, zaidi ya kunufaisha wawekezaji zaidi na watu wachache wanaohusika moja kwa moja na mchakato wa kuruhusu biashara hiyo.

Miongoni mwa wanaopinga hatua hiyo ya serikali ni Balozi Ali Abeid Karume, ambaye anadai kwamba "hakuna faida ya kukodisha visiwa vyoyote vya Zanzibar, kwani ni hatari zaidi kuliko kile kinachotazamiwa kuwa faida."

Ali Karume ambaye kitaaluma ni mchumi, aliyewahi kuwa Balozi wa Tanzania nchini Italia, hivi karibuni akiwa Unguja, alisema serikali inafanya makosa kukodisha visiwa hivyo, kwani kufanya hivyo kunaminya ustawi wa watu wa maeneo husika na kwamba faida inayozungumzwa na "wakubwa" haitakuwepo.

Balozi huyo anasema kwamba hata kiasi kinachotozwa wawekezaji wa kukodisha visiwa hivyo ni kidogo, ikilinganishwa na thamani ya ardhii na mazingira wanayokuta wawekezaji.

Anadai kwamba kila kisiwa, hasa vile vidogo, vinakodishwa kwa gharama ya Sh. milioni 240 (dola za Marekani 100,000) kwa mwaka, hata hivyo, Pambazuko limeelezwaa na kiongozi mmoja mwandamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwamba kiasi alichotaja Karume ni kidogo mno.

Baada ya kubanwa na Pambazuko ataje kiasi ambacho serikali inapata baada ya kukodisha visiwa, alikataa na kung'ang'ana kwamba – "achana na Ali



Balozi Karume

(Karume), hajui lolote, ye ye anapiga kelele tu. Amini tunapata fedha nyiningi mmo."

Balozi Karume anadai kuwa hata serikali ikodishe visiwa vyote 54 vya Unguja na Pemba (Zanzibar), bado faida haitaonekana kwa watu wengi, bali wachache.

Tayari Rais Mwinyi ametangaza kukodishwa kwa visiwa 17 ambayo vimepewa wawekezaji wa ndani na nje na kwamba serikali inafurahia uwekezaji huo wenye thamani inayofikia dola za Marekani milioni 400.

Pambazuko linazo habari kwamba baadhi ya visiwa viliviyokodishwa na thamani ya uwekezaji wake kwenye mabano ni pamoja na Changuu (dola milioni 20m); Bawe (milioni 30); Chapwani milioni 20); Chakware (milioni 68); Chumbe (uwekezaji unaendelea); Misali (milioni 83); Pamunda A na Pamunda B (milioni 30) na Pungume (milioni 10.5).

Dkt. Mwinyi anaeleza kwamba kukodishwa kwa visiwa hivyo kunatunisha mfuko wa maendeleo ya watu wa Zanzibar na kwamba wanaolaumu hatua huyo ya serikali wanashindwa kuelewa kwamba siyo mara ya kwanza kwa Zanzibar kuamua hivyo.

Rais huyo anasema Zanzibar itaendelea kukodisha visiwa vyake – vyenye sifa za kuperwa hadhi ya uwekezaji, ili kukuza ili kukuza uchumi wa buluu.

## Habari

### **SMCL kuboresha maisha ya waguswa**

Na Scovya MANASE

**K**AMPUNI ya Sotta Mining Corporation Limited (SMCL) inayomiliki mgodi wa dhahabu nchini Tanzania, imejipanga kuboresha maisha ya watu watakaoguswa na mradi wake.

SMCL yenyе hisa asilimia 84 na Serikali ya Tanzania kuwa na hisa 16, katika Mgodi wa Nyanzaga, imeweka bayana hatua za kuhakikisha watu watakaoguswa maeneo yao ya ardhi, mazao, maeneo ya biashara, watapewa stahiki zao kwa mujibu wa sheria za Tanzania na zile za kimataifa.

SMCL inajenga mradi wa dhahabu wa Nyanzaga katika vijiji ya Sotta na Nyabila, Kata ya Igalula, Wilaya ya Sengerema, Mwanza.

Mgodi huo unakadirwa kuwa na kiasi cha wakia 2.8 milioni za dhahabu.

Kuanza kazi kwa kampuni hiyo kunafuatia kupewe leseni na serikali ya uchimbaji mkubwa wa madini ya dhahabu mwaka 2021.

Mratibu wa kazi ya kuhamisha makazi na kulipa fidia wa SMCL, Paul Gongi ameliambia Pambazuko kwamba mahitaji ya ardhi kwa ajili ya shughuli za uchimbaji wa madini ni makubwa, na kwamba kila atakayeguswa atalipwa fidia stahiki.

SMCL katika kuhakikisha kila hatua ya utwajaaji wa ardhi na maeneo mengine unakenda sawa na kwa mujibu wa sheria, imetengeneza mpango kamambe wa kuwezesha zoezi lote linakwenda kama lilivypangwa na kuondoa kero na malamalikio kutoka kwa waguswa.

"Tumejipanga viliyvo, hatuna wasiwasi na kila mmoja atakayekuwa anaguswa na shughuli za mradi, tunapenda awe sehemu ya mafanikio ya SMCL," anaongeza Gongi.

Anasema kuwa taratibu zote za kuthaminisha ardhi, mazao na mali zingine zinazingatiwa na kwamba zitafanywa kwa ushirikiano mkubwa kati ya kampuni, waguswa, serikali na taasisi zote zinazotajwa na sheria ya utwajaaji ardhi.

Anasema kuwa SMCL imejipanga



**Waziri wa Madini Dotto Biteko**

kwa kutengeneza mfumo wa kina na shirikishi wa kuhamisha makazi na kaya zinazoguswa na mradi pamoa na kuhakikisha maisha ya waathirika yanaboreshwaa baada ya uhamisho.

Mbali na fidia, SMCL imejizitati kufuatilia maisha ya waguswa baada ya kuwa wamelipwa fidia, ili kuangalia namna wanavyoendesha maisha yao na ikiwezekana kuwapa ushauri wa namna mbalimbali za kisasa kuyaboresha.

Eneo la leseni ya mradi wa Nyanzaga linea kilometra za mraba 23.46 na linagusa vitongoji vitano ambavyo ni Sotta A, Nyang'hona, Kadashi, Kaningu B na Nyashimba ambapo linagusa kaya 725 na idadi ya watu 5,690.

Katika kuhakikisha kwamba wananchi wanaoguswa na miradi ya kimkakati wanalipwa fidia stahiki, hasa wale wa madini, mafuta na gesi, Serikali ya Tanzania imekuwa ikifuatilia kwa karibu na kushiriki kila hatua ili kila anayestahili fidia anaipata kwa mujibu wa sheria za Tanzania na hata zile za kimataifa.

## Habari

### 'Mbakaji wa Facebook' atiwa mbaroni

Na Mwandishi WETU,  
Arusha

**U**MAARUFU wa Jeshi la Polisi Tanzania unaendea kusambaa duniani kote baada ya kuonyesha uwezo na umahiri mkubwa katika kutenda kazi wake.

Sioo mara moja wala mbili, jeshi hilo la Polisi Tanzania limekuwa likipokea sifa kutoka maeneo mbalimbali duniani na hasa kwenye taasisi za kiusalama, ikiwamo Polisi wa Kimataifa (Interpol) kwa namna linavyofanya kazi kwa weledi – katika baadhi ya maeneo.

Ni kutokana na weledi huohuo, wiki iliyopita, Jeshi la Polisi limepongezwa kwa kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa wa jinai nchini Afrika Kusini ambaye alitoroka gerezani nam baadaye kutangazwa kwenye mitandao ya kijamii; Twitter na Facebook, kwamba amefariki dunia kwa kuchomwa moto.

Kumbe matangazo hayo ilikuwa ni mbinu ya kuzuia Polisi kumsaka kwa imani kwamba amefariki dunia – wakati ilikuwa uongo.

Rais huyo wa Afrika Kusini ambaye ni maarufu kwa tuhuma za makosa ya ubakaji na mauaji, alifanikiwa kutoroka kwenye gereza moja jijini Bloemfontein, Johannesburg na kujificha kwa muda kabla ya kutangazwa amefariki dunia.

Inaelezwa kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa kwa mara ya kwanza Julai, 2012 na kuhukumiwa kifungo cha muda mrefu kabla ya kutoroka Mei, 2021 na baadaye kutangazwa kufariki kwake dunia kupitia mitandao ya kijamii.

Thabo alikamatwa na kuhukumiwa baada ya kumbaka hadi kumuua mpenzi wake aitwaye Nomfundo Tyhulu – mwanadada huyu alikuwa mwanamitindo maarufu nchini Afrika Kusini.

Hata hiyo, vyombo vya usalama vya Afrika Kusini vilitilia shaka taarifa hiyo na kuentelea na uchunguzi wake na hatimaye Thabo Bester, alikamatwa Ijumaa iliyopita nchini Tanzania, katika Jiji la Arusha.



Thabo

Thabo alikamatwa na Jeshi la Polisi akiwa na mpenzi wake, Dkt. Nandipa Magumana na rafiki yake aitwaye Zakaria Alberto.

Thabo Bester ambaye anadaiwa kutumia mitandao ya kijamii, hasa Facebook kutongoza na hatimaye kufanikiwa kuwapata wasichana maarufu na wanafunzi na kuwabaka.

Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, David Misime amethibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo akiwa na mpenzi wake Dkt. Nandipa Magumana pamoja na raiwa mwagine Zakaria Alberto

Misime amesema taratibu za masasiliano ya kisheria ya Tanzania na mfumo wa kimataifa zinaendelea kukamilishwa ili kumrejesha mtuhumiwa huyo Afrika Kusini kwa hatua zaidi.

Jithada za kumkamata mtuhumiwa huyo zimefanikiwa zaidi kwa kutumia mfumo wake wa masasiliano ya simu ya mkononi ambapo pamoja na kuficha utambulisho wake, intelijensia ya idara kadhaa za usalama za Tanzania, Afrika Kusini na Polisi wa Kimataifa zikafanikiwa kumtua nguvuni.

Thabo ambaye mbali ya kudaiwa kuwa "mbakaji maarufu wa Facebook," pia anakabilwa na makosa mengine ya jinai, ikiwamo kutoroka gerezani, kudanganya kwamba amefariki wakati akijua kwamba haikuwa kweli.

## Kenya

# Ruto katikati ya mtego wa makamu wake

**Na Mwandishi MAALUM**

**M**AKAMU wa Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua ametishia "kubwaga manyanga" kwenye nafasi yake endapo mchakato aliouanza Rais William Ruto wa "kupatana" na mpinzani wake, Raila Odinga utafanikiwa.

Gachagua amesema kamwe hatakubali kubaki na nafasi yake, endapo Rais Ruto na Raila watakubaliana kushiriki – kwa namna yoyote ile, kugawana madaraka ya kuongoza Kenya.

Akizungumza katika Kanisa la AIPCA Limuru, Kaunti ya Kiambu, wiki iliyopita, Gachagua alisema kuwa iwapo ushirikiano na mapatano ya viongozi hao wenye wafuasi wengi nchini humo utafanikiwa yeeye "atakaa mbali."


Matamshi yake yanafuatia kuanza kwa mchakato wa viongozi hao kukubaliana kusitisha "minyukano ya kisiasa" ili kuwa na Kenya yenye amani na mandeleo.

"Ikiwa kutakuwepo na handisheki (makubaliano), mimi sitakuwepo. Mnajua kile hutoke kila wakati wa handisheki na Odinga. Mliona kilichomfanyikia aliposhirikiana na aliyekuwa kiongozi mmoja wetu aliyepewaa heshima. Mliona jinsi mambo yalivyoanza kuharibika," alisema Gachagua.

Kauli ya Gachagua iliungwa mkono na Gavana wa Kiambu, Kimani Wamatangi ambaye alisema kuwa ajenda ya handisheki haiwezi ikapigwa debe na Makamu wa Rais, Gachagua.

Wamatangi aliyekuwa akizungumza kwa kumpa sifa nydingi Gachagua – kwamba ni kiongozi shupavu na asiyeyumba katika misimamo yake, alisema kuwa kiongozi huyo hakika hatakuwa sehemu ya ushirikiao wowote utakaokubaliwa kwa viongozi hao wawili; Rais Ruto na Raila.

"Niliona meseji ya watu wa Odinga ikisema kuwa haweye akakubali handisheki na Gachagua. Msiwe na wasiwasi. Tunajua ni nini kilimfanya



*Gachagua*

afikirie tena. Hakuna mwanasiasa wanayeoropa kama wewe," alimpa sifa Gachagua.

Akaongeza, "Hii ni kwa sababu unapoanza kuongea, mambo huchukua mkindo tofauti, hivyo msitishiwe. Hakuna nusu mkate."

Kabla Rais Ruto kuchukua usukani, mtangulizi wake, Uhuru Kenyatta walikubaliana na Raila Odinga kuacha misuguano ya kiasi na kukubali kuwa na Kenya yenye umoja kupitia makubaliano yaliyopewa jina la "handisheki."

Ruto na Raila walikuwa wakiwania nafasi ya urais katika uchaguzi wa mwaka 2017, ambapo Uhuru alishinda, huku Raila akipinga ushindii wake kwa madai ya kuibwa kura. Msimamo wa Raila ulifanya Kenya kuwa taifa la maandamano na kukwamisha shughuli za maendeleo, hatua ambayo ilionekana kuweo kwa ulazima wa kushirikiana kwa wanasiisa hao na hatimaye kuleta amani nchini humo.

Hata hivyo, baada ya handisheki, wawili hawa wakawa marafiki wa dhati huku Rais Ruto ambaye wakati huo alikuwa makam wa rais akiwamua kuwa pembeni.



Na Evarist Chahali  
evarist@chahali.com

## Mezani kwa Chahali

### Samia ajipambanue kwa CAG

**W**IKI iliyopita, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) alikabidhi ripoti nyingine. Nimeandika "nyingine" kwa sababu hili ni tukio la kila mwaka.

Na japo sina tatizo na tukio hili kurudiwa kila mwaka, inafika mahala ambapo ni kama ripoti hizo siyo tu zinapoteza maana yake, bali pia zinatuongezea maumivu tunaoipenda Tanzania yetu kwa dhati.

Sina kumbukumbu kuhusu historia ya ripoti za CAG, kwamba lini zilianza kuwekwa hadharani, lakini ukweli ni kwamba mengi ya yanayobainishwa kwenye ripoti hizo huishia "kupuuuzwa."

Na hili la yanayobaishinishwa kwenye ripoti hizo kupuuuzwa yanachangia sana kushamiri kwa ujisadi katika Tanzania yetu. Kwa sababu, katika mazingira ya kawaida tu, kama kuna watu waliotajwa kwenye ripoti ya CAG ya mwaka 2021 – kwa kuhusika katika - ama matumizi mabaya ya madaraka au kuwa na dalili za ubadhirifu, lakini hawakuchukuliwa hatua, kwanini tutarajie waliotajwa mwaka 2022 wachukuliwe hatua?

Na kama wa 2022 hawakuchukuliwa hatua, kwanini tutarajie hawa waliotajwa majuzi wachukuliwe hatua?

Ujisadi unaongezeka kwa sababu hakuna utashi wa kisiasa kukabiliana na janga hilo na isiyokuwa bahati, janga hilo linaongezeka ukubwa na kuonekana linawashinda hata waliopewa dhamana kuzuia na kupambana na dudu hilo.

Na kweli ni janga haswa. Kwa sababu, kwa mfano, mionganii mwa yaliyobainishwa katika ripoti ya CAG ni ujisadi kwenye "fedha za Covid-19". Katika fedha hizo, dola za Marekani bilioni 1.6, sehemu kubwa ya fedha hizo ikiwa ni mkopo.

Hivi tuwe wakweli, katika mazingira tulionyayo ya umasikini wetu, ukichanganya na ujisadi unaokwapa



Rais Samia

hata kidogo tulichonacho, tutamudu kweli kulipa madeni kama hayo ya fedha za Covid-19?

Je, hatuwezi kufika mahala tukakumbuka tahadhari iliyotolewa na aliyekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri, Job Ndugai, kwamba tusipokuwa makini kwenye hiyo "kopa-kopa", nchi inaweza kupigwa mnada?

Wakati kuna ukweli kwamba kulikuwa na hadaa nyingi katika utawala uliopita, ambapo baadhi ya mashirika kama Shirika la Mawasiliano la Tanzania (TTCL) na Shirika la Ndege (ATCL), yalisifiwa kwa kuzalisha faida, yakafikia hatua ya kutoa gawio kwa serikali, lakini sasa infahamika kuwa yalikuwa yanazalisha hasara, serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ina wajibu wa kuweka hadharani udanganyifu uliofanyika huko nyuma.

Hatua hiyo itaweza kuisaidia serikali hiyo "kutobebeshwa lawama isizostahili." Waingereza wana msemo "huwezi kuila keki na ukabaki nayo", kwamba pindi ukila keki, lazima itaisha tu.

Serikali ya Rais Samia haiwezi kuendelea "kudumisha mazuri ya utawala uliopita" lakini hapohapo "ikajitenga na upungufu wa utawala huo."

## Habari

# Halmashauri watendaji wabovu

### Na Mwandishi WETU

**UTENDAJI** mbovu wa baadhi ya halmashauri na kutowapa wananchi huduma stahiki na kwa muda, kunaweza kubebwa na sababu anuai, lakini kubwa ni kuwa na viongozi wa idara wasiokwua na sifa.

Uchunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebainisha kuwa huduma zisizoridhisha kwa mamlaka za halmashauri za wilaya na miji, kunakwamisha ustawi wa kuhudumia wananchi inavyostahili.

Katika ripoti yake ya 2021-2022, CAG amebaini kuwepo kwa halmashauri mbili za Mkoa wa Iringa; Mafinga na Mufundi kuongoza kundi la halmashauri 106 kwa kuwa na viongozi 14 wa idara kila moja. Jumla ya wakuu wa idara 747 wabovu walibainika.

Katika mwaka wa fedha wa 2021 hadi 2022, Tanzania ilikuwa na Halmashauri 184. Hivyo, Halmashauri 106 zilikuwa na idara na vitengo ambavyo vinaongozwa na watumishi 747 wasio na sifa, ni sawa na asilimia 58.

Idadi hiyo ya kuwa na wakuu wa idara wengi – 14 kila moja, pia imebainika katika halmashauri za Babati, mkoani Manyara; Buchosa, Wilaya ya Sengerema, Mwanza; Hai, mkoani Kilimajaro na Ileje, mkoani Mbeya.

Pamoja na kwamba Ripoti ya CAG haielezzi kinagaubaga, sifa wasizokwua nazo wakuu hao wa idara. Pambazuko limebaini kuwa ni pamoja na kukosa elimu ya kutosha, uzoefu na hata weledi.

Tayari Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - Tamisemi), Angellah Kairuki amewaaagiza wakurugenzi kufuatilia na kuhakikisha kwamba nafasi zisizokwua na wakuu wa idara wenye sifa, zinajazwa haraka iwezekanavyo.

Kwa mujibu wa CAG, "idara na vitengo vinavyoongozwa na wafanyakazi wasio na sifa vinaweza kukabilwa na athari za utoaji wa huduma usioridhisha."

CAG anasema kuwa, halmashauri hizi zimekiuka maagizo ya Juni 16, 2022

yaliyozitaka mamlaka zote za serikali za mitaa kufuata na kutekeleza muundo mpya ulioidhinishwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa uchunguzi wake, hali hii ilitokana na changamoto za miingiliano ya majukumu ya wakuu wa idara na vitengo yaliyoinishwa kwenye muundo wa zamani kwenda kwenye muundo mpya.

Kwenye ukurasa wa 79 wa ripoti husika, CAG ameordodesha halmashauri zenye wakuu wa idara wasio na sifa.

Halmashauri hizo, na idadi ya watumishi wasio na sifa ikiwa kwenye mabano kwa kila Wilaya, ni kama ifatavyo:

Kuna Babati (14), Mbinga (10), Babati (11), Mbogwe (8), Bihamulio (11), Mbozi (10), Buchosa (14), Halmashauri ya Wilaya Mbulu (12), Buhigwe (11), Halmashauri ya Mji Mbulu (7), Halmashauri ya Mji Bukoba (6), Missemiyo (7), Halmashauri ya Wilaya Bukoba (6), Misungwi (7), Bukombe (2), Mkinga (4).

Zingine ni Busokelo (7), Mlele (5), Chato (6), Mombia (9), Chemba (4), Monduli (2), Chunya (8), Moshi (7), Geita (2), Moshi (3), Geita (1), Mpanda (3), Hai (14), Mpanda (1), Hanang (10), Mpimbwe (2), Ileje (14), Msalala (5), Illemela (7), Mtama (3), Iramba (6), Mtwara (7), Iringa (13), Mufindi (14), Iringa (12), Muleba (10).

Kadhaliika, kuna Kahama (7), Mwanga (4), Kakonko (9), Nachingwea (6), Kaliua (5), Namtumbo (14), Karagwe (4), Newala (9), Halmashauri ya Wilaya Kasulu (6), Ngara (5), Halmashauri ya Mji Kasulu (4), Njombe (7), Kibondo (3), Njombe (2), Kigamboni (2), Nsimbo (7), Kigoma (13), Nyanghwale (10), Kigoma-Ujiji (5), Nyasa (13), Kilolo (13), Rombo (10), Kilwa (6), Ruangwa (5), Kishapu (4), Rungwe (1), Kiteto (3), Same (8), Kondoa (4).

Pia, kuna Sengerema (10), Kondoa (1), Shinyanga (8), Kwigwa (8), Shinyanga (11), Kyela (1), Siha (8), Kyerwa (6), Simanjiro (14), Lindi (5), Songea (6), Liwale (7), Songea (5)na Ludewa (10).

## Watu Maarufu

### Ng'wanamalundi na miujiza yenye maswali mengi - IV

**Na Ibengwe Shileki MAZEYE**

**B**AADA ya ushindi wake, Mwanamalundi akaondoka Maswa na kwenda Kijiji cha Nela, Kwimba, Mwanza, ambako lilipangwa shindano jingine kubwa. Katika shindano hili Mwanamalundi alishinda. Kwa kuwa katika safari zake zote huambatana na jopo la wapishi wa chakula, ushindi huu ulimkwaza Gñđü Nkíma, mpinzani wake mkubwa ambaye aliamua kuloga chakula anachoandalua Mwanamalundi ili kisihi hata kikipikwa wiki nzima.

Ni kweli kabisa, wapishi wa Mwanamalundi walilalamika kuhusu chakula kutoiva kabisa kwa muda mrefu huku kuni zikiribia kuisha. Hivyo, wapishi wakaomba msaada wa kuni kwa Mwanamalundi. Baada ya wapishi kulalamika, Mwanamalundi akasonta/akanyoosha kidole kwene pori dogo jirani alipokuwa na kuwaambia wapishi waende wakakate kuni alikonyooshea kidole.

Isoyokuwa bahati, wakati ananyoosha kidole hicho hakujua kama ndani ya pori hilo kuliikuwa kuna mifugo na wachungaji kadhaa – watu wote pamoja na mifugo waliokuwamo ndani ya pori walikufa na kukauka kama kuni.

Tukio hili la kukausha miti na kuua ng'ombe na wachungaji wake, liliimuudhi sana kingozi wa Nela, Mtemi Masanja wa III ambaye aliamuru askari wake waende kumkamata Mwanamalundi haraka iwezekanavyo ili awajibishwe.

Askari wa Mtemi Masanja waliogopa sana kumkamata Mwanamalundi wakihofia kufa, hata hivyo amri ya Mtemi haipingwi, hivyo Iliwalazimu kwenda kumsaka na kumkamata tu sababu walimuogopa zaidi kiongozi.

Kabla Mwanamalundi hajakamatwa, inaelezwaga kwamba alijua jambo hilo lingetokea. Hivyo akaenda haraka kumuaga mama yake mzazi na



*Mwanamalundi*

kumuchchia maagizo. Mwanamalundi alikamua maziwa kiasi fulani kwenye kikombe na kisha akampa mama yake na kumwambia; "Iwapo maziwa haya yataanza kuganda, ujue kuwa niyo katika halii mbaya, iwapo yataganda kabisa, ujue kuwa nimekuwa!"

Mwanamalundi akachukua shoka isiyo na mpini kisha akaiegamisha ukutani na kumwambia mama yake, "Iwapo nitakamatwa na kupelekwa kuuawa, shoka hii itakuwa ikipanda ukutani nikwiwa naapelekwa kukatwa shingo, tukifika eneo nitakalouawa, basi hii shoka itapandisha hadi mwisho wa ukuta kuonesha kuwa tumefika mwisho wa safari!" Mama yake alipokea maagizo hayo na haikuchukua muda Mwanamalundi akakamatwa na askari wa Mtemi Masanja.

Mtemi Masanja III aliamua kupeleka shauri hilo kwa watawala wa kikoloni (Wajerumanii) ili wamchukulie hatua Mwanamalundi. Uchunguzi ukafanyika na Mwanamalundi akaonekana ana hatia ya mauajji ya watu wasio na hatia. Adhabu ya kosa hili ilikuwa ni kunyongwa.

Katika safari hii ya kunyongwa, Mwanamalundi aliambatana na Makongoro Igana ambaye alikuwa ni Mtemi wa Ilemela. Mtemi huyu alikuwa ana hatia ya kuwachapa viboko Wajerumanii baada ya kupita eneo ambalo hawakuruhusiwa wageni.

Mtemi Makongoro Igana kila alipokuwa akisafiri juu ya punda, mkono wake wa kuume ulikuwa umeshika fimbó

## Watu Maarufu

# Ng'wanamalundi na miujiza yenye maswali mengi - IV

**Inatoka Uki.**

ndefu. Fimbo hiyo hutumika kumchapia kila atakayepita upande wa kuume katika safari zake.

Wajerumani hawakujua utaratibus huo wa Mtemi Makongoro. Siku wajerumani walipopishana safarini na Mtemi Makongoro, walipita upande wa kuume wenye fimbo. Mtemi Makongoro akawachapa fimbo wazungu hao kama ilivyo jadi yake. Wazungu hao walishindwa kumvumilia, wakamkamata na kumfungulia mashtaka yaliyoamuru anyongwe.

Mtu mwininge akitiwa Kaliyaya, aliyambatana na Mwanamalundi katika safari ya kunyongwa. Huyu Kaliyaya alikuwa ni mtu aliyeonekana ni mwene ushawishi mkubwa kwa watu wa jamii yake. Kukubalika kwake kulimfanya apate wafuasi wengi amba walihofiya kumpindua Mjerumani. Hivyo wajerumani wakaona ni bora wamfungulie mashtaka ili wamnyonge kabla hajawapindua.

Kaliyaya alikuwa ni mtu wa kawaida tu ila ni mwene ushawishi na kipenzi cha watu wengi.

Mtu wa tatu aliyeambatana na Mwanamalundi katika safari ya kunyongwa ni Mtemi Italange wa Bugando. Mtemi huyuалиngia mgogoro na Wajerumani baada ya kuhodhi eneo kubwa la pwani ya Žiwa Victoria na bandari zake kisha akakataa kuwapa Wajerumani. Ili kumnyang'anya utajiri huo, Wajerumani wakaamua kumfungulia mashtaka ili wamnyonge.

Zoezi la kunyongwa lilipofika, Mwanamalundi alikuwa ndio mtu wa kwanza kuvishwaa kitanzu. Kamba ilipofiyatuliwa tu ili kumuua, kamba ikakatika yenye. Zoezi la kumuua likaahirishwa, badala ya kunyongwa akababalishiwa adhabu.

Ikaja zamu ya Mtemi Makongoro Igana. Mtemi alipowekewa tu kitanzu

shingoni na kisha kuifyatua kamba hiyo ili kumuua, ghafla kukatokea mfano wa sinema kwenye ukuta. Ni sinema ya kimiujiza iliyoonesha matukio ya kivita miaka ya nyuma.

Askari wakageuka kuitazama sinema hiyo. Sinema haikuchukua zaidi ya dakika moja, ikaisha. Walipomgeukia yeye (Mtemi Makongoro Igana) wakaona hana kamba shingoni. Huyu naye akawekwa pemberni na kubadilishiwa adhabu.

Akaja Mtemi Italange. Huyu alipowekewa kitanzu shingoni, naye pia kamba ilifyatuka. Akawekwa pemberni na kubadilishiwa adhabu. Ilipofika zamu ya Kaliyaya, kitanzu kilipofiyatuliwa ili kumnyonga, hakika kitanzu kilimuua. Huyu hakuwa mwene ulinzi wowote ule kishirikina; yaani alikuwa ni mtu wa kawaida tu.

Ndipo mamlaka za Wajerumani ikaamuru askari wapeleke watu hao watatu Tabora kutoka Mwanza. Wakiwa njiani kuelekea Tabora, walifika Nzega na kuamua kupumzika kidogo chini ya mti mkubwa nje ya Shule ya Sekondari Chama.

Hapo askari wa utawala wa Wajerumani wakaendelea kuuliza maswali mengi kwa Mwanamalundi kuhusu nguvu zake na kisha wakamuomba afanye muujiza wa mwisho kabla hajafikishwa gerezani.

Mwanamalundi akawaambia askari kuwa bado ana uwezo mkubwa, hata huo mti walipomzikia anawenza kuauasha. Aliongea maneno hayo huku akiupigapiga mti huo, ghafla mti ulikauka palepale na majani makavu yakaanza kudondoka. Askari wale waligopa sana tukio hilo.

Walipofika Tabora Mjini, Mwanamalundi na wale watemi wawili walipelekwa gerezani ambamo walijunganishwa na watu wengine wenye makosa yaliyoitwa "makubwa" kisha baada ya siku kadhaa wakapelekwa Kisiba cha Mafia, Pwani ili kutumikia kifungo cha miaka mitatu.

## Waafrika mamboleo na maadili asilia

Na Digna DESIRATA

**W**AAFRIKA wengi, chini ya uongozi wa machifu wao walipinga utumwa, ubaguzi na utengano uliokuwa unasababishwa na wakoloni.

Badala yake walihimiza uhuru, usawa na umoja wa binadamu wote, bila kutofautisha kati ya wagensi na wenyeji.

Misimamo ya Waafrika hawa ilitokana na uelewa wao, kama Waafrika, kuhusu nadharia ya maadili asilia, ambayo msingi wake ni “kanuni ya usawa wa kimaumbile” kati ya watu wote.

Mfano, kuhusu maadili, mwanafilosofia Tempels (1959:56), katika kitabu chake cha “Bantu Philosophy,” anasema kuwa, “Maadili ya Wabantu hukataza uwongo, ulaghaji, wizi na uzinzi, kutokana na sababu zilezile za uharibifu dhidi ya ustawi wa watu unaotokana na tabia hizi.”


Anaongea kuwa, maadili ya Wabantu “pia yanakataza, kwa mtazamo wa Kibantu, tabia kadhaa kama ndoa za utotonu, na ukatili wa kijinsia.”

Anahitimisha kwamba, “kwa ufupi, Wabantu wanajua na kukubali sheria asilia ya maadili kama inavyofanuliwa kuititia Amri Kumi za Musa.”

Inapswa kuangalia mtazamo wa Waafrika kwa msaada wa fikra za Wanazuoni Mamboleo wafuatao, walioandika kuhusu maisha ya Afrika:

Placide Tempels (1959) na kitabu chake, “Bantu Philosophy”; John Mbiti (1969) na kitabu chake, “African Religion and Philosophy”; Barry Hallen (2002) na kitabu chake, “A Short History of African Philosophy”; Kwasi Wiredu (2004) na kitabu chake, “A Companion to African Philosophy.”

Na wengine wakiwamo John Iliffe (2007) na kitabu chake, “The History of a Continent”; Molefi Asante na Ama Mazama (2009) na kitabu chao “Encyclopedia of African Religion”; Elvis Imafidon na John Bewaji (2014) na kitabu chao, “Ontologized Ethics”; Isaac



Tempels

Ukpoko (2017) na kitabu chake.

Pia, “Themes, Issues and Problems in African Philosophy”; Ademola Fayemi (2017) na makala yake, “African philosophy in search of historiography”; na Motsamai Molefe (2019) na kitabu chake, “An African Philosophy of Personhood, Morality, and Politics”. Ufafanuzi wa vitabu hivyo ni kama ifuatavyo;

Jawabu kwa swali la kiteolojia

Kuhusu swali la kiteolojia linalouliza, “mpango wa Mungu wa dini yetu unasema nini kuhusu maisha bora na ustawi thabiti wa kila mtu,” majibu ya Waafrika mamboleo ni haya:

Kwamba, inawezekana kuwa kanuni za maumbile, tunazozikubali kwa kauli moja, zilitoka kwa Mungu fulani, japo hatukubaliani kwa kauli moja ni Mungu yupi amesanifu kanuni zipi, lini na kivipi;

Kwamba, ubaya wa tabia kama vile wizi hautokani na tamko la kimungu, bali tamko la kimungu ni njia ya kutufahamisha ukweli kwamba, tabia hiyo inapingana na kanuni ya ustawi wa watu;

Na kwamba, kwa hiyo, hata bila kujuliza kanuni za maumbile zimetoka

## Uchambuzi

### Waafrika mamboleo na maadili asilia

*Inatoka Uk. 13*

wapi, tunaweza kujadili na kukubaliana kuhusu kanuni za maadili asilia kutokana na kanuni za maumbile pekee bila kuongelea kanuni za ufunuo wa kimungu.

Jawabu kwa swali la kibayolojia

Mbili, kuhusu swali la kibayolojia linalouliza, "binadamu ni kitu chenye hulka ya namna gani endapo hulka yake itatazamwa kama mti wenyewe matawi mbalimbali," majibu ya Waafrika mamboleo ni haya:

Kwamba, kuna tofauti kati ya mtu na kitu, tofauti kati ya utu na ukitu.

Kwamba, kila binadamu ni kiumbehai chenye mwili uliogawayika katika viungo mbalimbali vinavyotofautiana, na vyenye kukamilishana kikazi, kila kiungo kikiwa na silika asilia ya kibayolojia inayokielekeza namna ya kutekeleza kazi yake.

Kwamba, kila kiungo cha mwili kinapigania uzima na ustawi wa mwili mzima, lakin chini ya usimamizi wa kiungo cha mwili kiiwtacho "ubongo," ambacho ni kitovu cha hazina ya akili na utashi.

Kwamba, kuna silika asilia za kibinadamu nydingi, baadhi zikiwa na sura chanya, zingine sura hasi.

Kwamba, kwa upande mmoja, kuna silika asilia ya kupenda miguu minene (eruophelia), kupenda matiti yaliyotuna (lactophilia), kupenda macho makubwa (oculophilia), kupenda nywele ndefu (tricophilia), kupenda kufanya mapenzi (erotophilia).

Pia kupenda umati (agoraphobia), kupenda mtu wa jinsia tofauti (heterophobia), kupenda mtu wa jinsia moja (homophobia), kupenda watoto (pedophilia), kupenda wazee (gerontophobia), na kupenda ugomvi na hata kupenda maiti (necrophilia).

Kwamba, kwa upande mwininge, kuna silika asilia ya kuogopa kufanya mapenzi (erotophobia), kuogopa umati (agoraphobia), kuogopa mtu wa jinsia tofauti (heterophobia), kuogopa mtu wa jinsia moja (homophobia),



**Robert Moffat**

kuogopa watoto (pedophobia), kuogopa wazee (gerontophobia), kuogopa maiti (necrophobia), kuogopa kinyesi (scatophobia).

Kwamba, baadhi ya silika asilia chanya zilizotajwa hapo juu ni viashiria asilia kwa ajili ya kumwonyesha kibindamu malengo yenye mchangi chanya katika ustawi wake.

Na kwamba, baadhi ya silika asilia hasi zilizotajwa hapo juu ni mbinu ya kibindamu ya kulinda na kukuza maisha yake dhidi ya hatari za kimazingira.

Jawabu kwa swali la kisaikolojia

Tatu, kuhusu swali la kisaikolojia linalouliza, "kuna uhusiano gani kati ya fikra, maamuzi na matendo ya kibinadamu," majibu yao ni haya:

Kwamba, wanadamu ni "viumbe wenyewe urazini," yaani uwezo wa kutumia ubongo kufikiri, kukumbuka, kutambua, kuamua na kufanya matendo huru ya kimwili chini ya uongozi wa ubongo, matedu haya yakiwa ni mbinu ya kufanikisha lengo kuu la maisha binafsi na ustawi wa jamii.

Tangazo

## Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoe  
huduma, endapo unahitaji kuwafikia  
wateja wengi zaidi bila kujali mipaka  
ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha  
na kupambazua huduma na  
biashara yako.

*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au Barua-  
Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

**Pambazuko**

Namba 33

Jumatatu April 3

Uk.  
10-11

**Wiz  
wiz**



## Historia

### Kesi dhidi ya Yesu ilivunja sheria

**Na Mwandishi MAALUM**

**M**AADHIMISHO ya Sikukuu ya Pasaka, yamechanganyika katika maeneo mawili; huzuni na furaha.

Katika huzuni, kiongozi wa Wakristo, Yesu aliyezaliwa zaidi ya miaka 2,000 iliyopita katika mji mdogo wa Bethlehemu katika nchi ya Yudea, alikamatwa, akateswa na hatimaye kuuawa.

Lakini historia hiyo hiyo, inaeleza upande wa pili wa Pasaka, kwamba baada ya kuuawa na kuzikwa, Yesu alifufuka na kuwa ishara ya ukombozi na kufutwa kwa dhambi kwa wale wanaoamini.

Kabla ya kuuawa kwa Yesu Kristo, Mnazaileth, kulikuwa na mchakato wa kesi ili kumtia hatiani na hilo lilifanywa ili kuhakiisha kwamba "haki inaonekana na inatendeka."

Kesi ya Yesu Kristo hadi kuhumiwa kifo ilipita katika sehemu sita katika uendeshaji wake katika mahakama mbili; Mahakama ya Kidini (Kiyahudi) na Mahakama ya Kisiasa (Kirumi).

Na katika Mahakama hizi zote mbili, mashitaka yalikuwa tofauti kulingana na makosa yaliyoletwa kwenye mahakama husika.

Katika kila mahakama, kulikuwa na hatua tatu kama ifuatavyo; Mahakama ya kidini – yesu aliwekwa mbele ya kionogi aitwaye Anasi, baadaye akapandishwa kizimbani mbele ya Kayafa na mwisho kwenye Baraza.

Katika Mahakama ya Kidini ya Kiyahudi, Yesu alishtakiwa kwa Makosa Mawili; kukufuru (alisema atalivunja hekalu na kujilenga kwa siku tatu, hii iliwa kufuru) na pia kujiita Mwana wa Mungu (Masiya).

Makosa yote hayo yalikuwa ni makosa ya kidini na alitakiwa aadhibiwe kwa taratibu za kidini katika mahakama hiyo.

Lengo la viongozi wa kidini ya Kiyahudi liliwa ni lazima Yesu afe kwa sababu walimwona kuwa mwiba kwenye maslahi yako.

Kwa vile Mahakama ya Dini ya Kiyahudi haikuwa na mamlaka ya kutoka



*Picha ya kuchora inayoaminika kuwa sawa na sura ya Yesu*

hukumu ya adhabu ya kifo hasa wakati wa utawala wa Warumi kule Palestina (pamoja na Israeli), viongozi hao wa dini wakaamua kumpeleka Yesu kwenyne Mahakama ya Kisiasa (Kirumi) kwa Ponsio Pilato ambaye alikuwa Gavana akimwakilishi Kaisari.

Pilato ndiye aliyekuwa anasimamia mahakama hiyo ya Kirumi na ndiyo iliyokuwa na mamlaka ya kumhukumu mtu adhabu ya kifo.

Katika mahamaka ya Kisiasa, shauri la Yesu ilipita katika hatua tatu; alisimama mbele ya Pilato, Herode na Pilato tena kwa hukumu ya mwisho.

Viongozi wa Dini ya Kiyahudi ndio waliokuwa walalamikaji (Washitaki). Walielewa kuwa wakienda kwa Pilato na yaleyale makosa au mashtaka ya kidini, Pilato atawaambia wakamhukumu kwa sheria zao za kidini.

Kwamba hata kama angeamua kutoa hukumu, basi hukumu hiyo isinge kuwa ni adhabu ya kifo (kama ambavyo wao walitaka Yesu auawe).

Kutokana na sababu hizo, wakaamua kuyabdalisha mashtaka yake kutoka makosa ya kidini na kumbambikizia makosa ya kisiasa.

Hapo kwa Pilato wakaja na makosa  
*Endelea Uk. 17*

## Historia

# Kesi dhidi ya Yesu ilivunja sheria

Inatoka Uki. 16

matatu; kuwataharakisha watu (kuwachochea watu wagome na kuupinga utawala wa Kirumi wa Kaisari - hili ni kosa la uchochezi); kuwakataza watu wasilipe kodi kwa Kaisari na kujifanya yeze ni Mfalme (dhidi ya Kaisari).

Makosa hayo yote kimsingi ni makosa ya uhaini na adhabu yake ni kuhukumiwa kifo.

Pamoja na hila zote hizo, bado walikosa ushahidi wa kumshawishi Pilato atoe hukumu hiyo. Pilato akaitupilia mbali hii kesi kwa sababu ilikosa hoja za kimantiki katika sheria. Akawaambia wampeleke Herode shauri hilo kwa kuwa Yesu alikuwa raia wa eneo la Galilaya na Herode (Antipas) alikuwa mtawala wake wa kimila.

Herode ambaye alikuwa Yerusalemu kipindi hicho cha Sikukuu ya Pasaka, naye hakuona kosa lolote la Yesu. Zaidi alifurahi tu kumwona maana alikuwa anazisikia tu habari zake akiambiwa na watu; na alikuwa anamchanganya na Yohane Mbatizaji.

Herode hakutaka kuendelea na kesi hiyo na akashauro wamrudishe tena kwa Pilato huku wakishinikiza kwa nguvu zote na kelele kuwa asipomhukumu Yesu adhabu ya kifo maana yake hana ushirika na Kaisari. Na pia watamtaarifu Kaisari kuwa Pilato anawatetea watu wanaompinga Kaisari.

Pilato aliposikia hayo na kwa kuogopa "kutumbuliwa" na Kaisari akaamu kufanya kama walivyotaka. Akamhukumu Yesu adhabu ya kifo kwa kuwambwa msalabani chini ya usimamizi wa askari wa Kirumi.

Taratibu za kisheria zavunjwa

Kesi ya Yesu ndiyo intajwa kuongoza mpaka sasa kwa kuvunja rekodi ya uvunjifu wa taratibu nyngi za mshingi wa kisheria katika shughuli za uendeshaji wa mashtaka.

Rekodi hii hajjawahi kuvunjwa hadi sasa na hili linawenza kuthibitishwa na hatta zifuatazo;

Baada ya Yesu kukamatwa alitakiwa

apelekwe kwenye gereza lililokuwa ndani ya hekalu mpaka hapo Baraza Kuu la Wayahudi litakapokaa kama ambavyo Mitume Petro na Yohane walivyowekwa (Matendo 4:3; 5:17), lakini Yesu mara tu baada ya kukamatwa akapelekwa nyumbani kwa Kuhani Mkuu (Yohane 18:13-27).

Hii ilikuwa tofauti au kinyume na taratibu za kawaida; kwanza kilikuwa ni kipindi cha Pasaka. Usiku huo ulikuwa ni Usiku Mtakatifu kadili ya Litrurija ya Wayahudi, na makuhani walitarajiwu kuwa na familia zao na siyo kusikiliza kesi ya Rabu ti fulani kutoka Galilaya.

Pili, nyumba ya Kuhani Mkuu kwa vyovoyote vile ilikuwa nzuri na ya kistarehe kiasi kwamba pengine isingeweza kuwatoshwa wajumbe wote 72 wa baraza hilo kama wangeweza kukusanyika wote kwa taarifa ya haraka na ya muda mfupi kiasi hicho.

Pia haikuruhusiwa kesi au shauri lolote kuendeshwa wakati wa Sikukuu au Maandalio ya Sikukuu, lakini viongozi haohao wa sheria za Kiyahudi waliendesha shauri la Yesu wakati wa Sikukuu ya Pasaka.

Kila mjumbe wa Baraza alipaswa kupiga kura binafsi/kwa siri kukubali au kukataa wakati wa uamuzi wowote ya hukumu, lakini Yesu alihukumiwa kwa



Endelea Uki. 18

## Historia

### Kesi dhidi ya Yesu ilivunja sheria

*Inatoka Uk. 17*

kura ya pamoja.

Kama mtu akihukumiwa kifo huko Rumi, hukumu hiyo ilitakiwa itekelezeza siku inayofuata, lakini Yesu alihukumiwa na hukumu hiyo ilitekelezeza muda mfupi tu baada ya kutolewa.

Wayahudi hawakuwa na mamlaka ya kutoa hukumu ya kifo, lakini hukumu ya Yesu ilipendekezwa na Wayahudi na wakampeleka kwa Pilato kuomba ruhusa ya utekelezaji.

Haikuruhusiwa shauri lolote kuendeshwa wakati wa usiku, lakini shauri la Yesu liliendeshwa usiku.

Mtuhumiwa yejote alipaswa kupewa mshauri au wakili na uhuru wa kuleta mashahidi, lakini Yesu hakupewa nafasi hii ili kuhakikisha adhabu wanayoitaka wahiaki, itolewe bila kipingamizi.

Mashtaka ya mtuhumiwa yalipaswa kubakia hayohayo katika kila hatua ya kesi, lakini mashtaka ya Yesu yalibadilika kila hatua ya kesi kutoka kukufuru na kujijita yeye ni Mwana wa Mungu (Masih) alipopelekwa kwenye Mahakama ya Kidini, hadi kutaharakisha jami na kusababisha uasi, kuwakataza watu kulipa kodi kwa Kaisari na kujitangaza kuwa ni Mfalme wa Wayahudi.

Mtuhumiwa hakutakiwa kuulizwa maswali ya kujifunga au maswali ambayo majibu yake yatamfunga, lakini Yesu aliulizwa kama yeye ni Kristo.

Yesu hakuwa na kosa

Kuna mazingira kadhaa yanaonesha Yesu alihukumiwa bila kosa kuanzia mwanzo kesi hadi mwisho.

Zipo dalili zilianza kujitokeza mapemba kwamba Yesu hakuwa na makosa na hilo lilimtokea mke wa Pilato ambaye alioteshwa katika kuwa Yesu hakuwa na hatia na akamtumia ujumbe huo mumewewe (Matayo 27:19)

Pilato alijitahidi sana kuepuka kumhukumu kifo Yesu. Kulikuwa na desturi ya kumfungua mfungwa mmoja wamtakaye kipindi cha Sikukuu ya Pasaka (kama tu ambavyo rais wan chi anatoa msamaha kwa wafungwa kipindi



*Yesu amefufuka*

cha Sikukuu ya Uhuru), Pilato alijaribu kuitumia desturi hiyo ili aweze kumtoa Yesu.

Akaamua kuwalettea Baraba, mtu mharifu na aliyeleta taharuki kwa kuleta kile kilichoelezwa kuwa ni fitina na kusababisha mauaji, hivyo akampeleka mbele ya umma na kuuliza nani aachiwe huru kati ya Yesu au Baraba? Aliamini kwamba watamchagua Yesu atoke na Baraba ahukumiwe, lakini wakataka afunguliwe Baraba na Yesu asulubiwe (Matayo 27:15-18).

Pilato alijaribu sana kuuliza umma uliokusanyika kutaka kujua kosa hasa la Yesu ni lipi hadi kustahili kusulubiwa - akawauliza, "kwani ni ubaya gani aliooutenda?" (Matayo 27:23); bado wakajibu, "Na asulubiwe."

Mwisho, Pilato akaamua kuosha mikono yake kuonesha kuwa yeye hana hatia juu ya kifo cha Yesu. Akasema, "mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenywewe" (Matayo 27:24). Kwa kulinda cheo chake kama Gavana akamtoa Yesu kwao asulubiwe.

## Ndondi



# Mwakinyo kuzichapa Dodoma

APRILI 23 ngumi zitapigwa sana tu jijini Dodoma wakati bondia maarufu nchini, Hassan Mwakinyo atakapopanda ulingoni kuzipiga na Kuvesa Katembo wa Afrika Kusini.

Lengo la pambano hilo ni kusaidia kupata pesa za kununua taulo 40,000 za watoto wa kike ambazo zitagawiwa kwa wanafunzi wa mikoa wa nyanda za juu Kusini.

Tayari kampuni ya Softcare Sanitary Pads imetoo taulo 20,000 na fedha ambavyo kwa pamoja vina thamani ya Sh. milioni 35 ili kuunga mkono juhudhi hizo kwa mabinti hao.

Promota wa shindano hilo, Sophia Mwakagenda, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, alisema katika kuona umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike waliamua kuandaa pambano hilo ili kuchangia taulo za kike ziweze kuwasaidia mabinti kuondoa vikwazo kwenye masomo yao.

Promota huyo alitaja sababu kuchagua pambano hilo kufanya Aprili 23, Dodoma ni kuhakikisha idadi kubwa ya wananchi wanapatikana kushuhudia masumbwi hayo kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania.

“Kwa kuwa Dodoma ni katikati ya nchi, tunatarajia watu wengi zaidi kutoka mikoa ya jirani watahudhuria, lakini kwa sasa Dodoma vikao vya Bunge viinaendelea, hivyo ushiriki wa wabunge ni muhimu sana na wanawea kupatikana kwa urahisi kwa sasa,” alisema mbunge hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa Dorrycare Technology Company, Victor Zang alisema lengo la pambano hilo ni kuchangisha fedha za kununua angalau taulo za kike 40,000 na kuzipeleka kwenye jamii, hususani kwa wanafunzi na wanawake wenye mahitaji maalumu ili kuwashakikisha hedhi salama.

**Mwanaspoti**

# **POLE SANA MWANJILE...**



*Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia) akizungumza kwa kumfariji Brigedia Jenerali (mstaafu) Aloyce Mwanjile juzi - Jumamosi; Aprili 8, 2023, alipokwenda Bunju A, Dar es Salaam kuhani msiba wa binti wa Mwanjile, Faithnancy, aliyefariki Ijumaa - Aprili 7, 2023. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

